NEW

# DOKEZO SABILI

THRO
Endelea ya taratibu
TD 10/10/2022

**KWENDA KWA:** Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji,
**MASASI.**

**TAREHE:** **10/10/2022**

**YAH: NAFASI WAZI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA.**

Tafadhali naomba urejee somo tajwa hapo juu,

Kufuatia kifo cha aliyekuwa Mwenyekiti wa bodi ya **Ajira** katika Halmashauri ya mji masasi ndugu,**Thomas Kambelenje** kilichotokea tarehe **10/11/2017**, ilipelekea kuwepo kwa nafasi wazi ya Mwenyekiti wa bodi ya ajira katika Halmashauri ya Mji masasi.

Aidha kwa kuzingatia Kanuni za utumishi wa Umma za Mwaka 2003, **Kanuni Na.130 (2)** Ofisi yako kupitia baraza la Madiwani, ilifanikisha zoezi la kuteuliwa kwa ndugu, **Mtombo Omary Lilibe** ili kuziba nafasi ya **Mwenyekiti** wa bodi ya Ajira kwa kipindi cha Miaka miwili iliyokuwa imesalia kuanzia **Tarehe 01/07/2018** hadi **Tarehe 01/07/2020.**

Baada ya kupitia **Sheria,Kanuni,Taratibu** na **Miongozo** mbalimbali ya utumishi wa Umma inayohusu uendeshaji wa **Bodi**, pamoja na nyaraka mbalimbali zilizomo kwenye faili la **Bodi** ya ajira nimebaini kuwa **Mwenyekiti** huyo **Mteule** ameendelea kutumikia nafasi hiyo **Kimakosa** kwani muda wake wa kisheria uliishia Tarehe **01/07/2020,** hivyo kwa kuzingatia kanuni za utumishi wa Umma za mwaka 2022, napendekeza mambo yafuatayo ili kutatua dosari hii:-

1. Kutumia Kanuni za utumishi wa Umma za mwaka 2022, **Kanuni Na.119,** ikisomwa pamoja na **Kanuni Na. 117(1b),** ili kuruhusu shuguli za bodi yetu ya ajira kuendelea na shughuli zake bila kumtumia **Mwenyekiti mteule** ambaye alipaswa kuhitimisha muda wake **Tarehe 01/07/2020** kwa barua yenye **KUMB.NA.MTC/B.10/3/67** ya **Tarehe 09/07/2018**, kwani kanuni hizo kwa pamoja zinaelekeza kuwa **Bodi** inaweza kuendelea na shughuli zake hata kama kutakuwa na **ombwe** la mjumbe ,aidha mmoja wa wajumbe wa bodi anaruhusiwa kuziba nafasi ya Mwenyekiti wa bodi ya ajira kwa mujibu wa **Kanuni Na.117(1b) ya kanuni za utumishi wa Umma za mwaka 2022.**

2. Kutekeleza **Matakwa** ya **Kanuni Na. 113(1)** ya kanuni za utumishi wa umma za mwaka 2022 kwa kutangaza nafasi wazi ya **Mwenyekiti Wa Bodi** ya ajira ili kuziba nafasi ya Mwenyekiti aliyemaliza muda wake wa miaka miwili mnamo tarehe **01/07/2020.**

Sambamba na maelezo hayo napenda kufafanua kuwa shughuli zote zilizotekelezwa na **Bodi** kwa kumtumia **Mwenyekiti** aliyetakiwa kuhitimisha muda wake **Tarehe 01/07/2020** hayataathiriwa kwa vyovyote vile na utekelezaji wa mapendekezo haya kwani shughuli za **Bodi** na maamuzi yake yamelindwa kwenye **Kanuni Na.119** ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022.

Naomba kuwasilisha kwa ridhaa yako,

**JUMANNE CHAULA,**
Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi,
Halmashauri ya Mji,
**MASASI**

NEW

NEW

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI MASASI

*(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi wa Mji)*

**Kumb. Na. MTC/L.10/1/VOL V/02** **Tarehe:** 10/10/2022

# TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi kwa kuzingatia kanuni **Na.113 (1)** ya kanuni za utumishi wa umma za mwaka 2022, anawatangazia watanzania wote wenye sifa, kuomba nafasi ya **Mwenyekiti** wa bodi ya ajira baada ya bodi ya awali kukamilisha kipindi chake cha Uongozi.

1. SIFA ZA MWOMBAJI

a) Awe **Raia** wa Tanzania.
b) Awe **MKAAZI** wa kudumu katika eneo la Kiutawala la **Halmashauri ya Mji Masasi**.
c) Asiwe **ameajiriwa** au **Mtumishi** wa Umma.
d) Awe na **Umri** kuanzia miaka 45 na kuendelea.
e) Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea.
**f)** Awe na uelewa katika fani za **Usimamizi** wa **Rasilimali Watu**,**Utawala wa Umma au Sheria.**
**g) Awe na uzoefu wa Uongozi.**

2. KAZI NA MAJUKUMU YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA.

- **Jukumu** kubwa la **Mwenyekiti wa bodi** ya **Ajira** ni kuongoza Vikao vyote vya kisheria vya bodi ya **Ajira** ambavyo ni;

a) Kikao cha Kuajiri **watumishi wapya.**
b) Kikao cha **Kuwathibitisha kazini** watumishi wa **Ajira mpya**/waliopanda vyeo.
c) Kikao cha **Kupandisha Vyeo /Kubadilisha Vyeo vya Kimuundo** kwa Watumishi waliojiendeleza kielimu.

**MALIPO:**

Kazi ya **Mwenyekiti** wa **Bodi** ya ajira **haina mshahara** isipokuwa **atalipwa Posho ya Kikao** kwa mujibu wa **miongozo/nyaraka za Posho kwa** watumishi wa Umma.

NEW

NEW

**MASHARTI YA JUMLA.**

(i) Waombaji wote waambatanishe vyeti vya shule na Taaluma na cheti cha kuzaliwa (Certified Copy).

(ii) Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza "CV" yenye namba za simu za wadhamini.

(iii) Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

(iv) Uwasilishaji wa sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria

(v) Maombi yote yapitie kwa Mtendaji wa Mtaa/ Kijiji husika.

**NB: Waombaji wote mnatahadharishwa kujiepusha na matapeli wanao jitambulisha kuwa wao ndio waajiri na kukutaka utoe Rushwa.**

Maombi haya yawasilishwe kuanzia Tarehe **10/10/2022** hadi **17/10/2022** saa **9:30 alasiri**.

**MAOMBI YOTE YATUMWE KWA ANUANI IFUATAYO**

MKURUGENZI WA MJI,
HALMASHAURI YA MJI MASASI,
S.L.P 447,
**MASASI.**

Elias R. Ntiruhungwa
Mkurugenzi wa Mji
**MASASI**

MKURUGENZI WA MJI MASASI
S. L. P 447
MASASI

NEW